

Pambazuko

Toleo Namba 052

Jumatatu Novemba 6-12, 2023

Uk. 6



CCM, Chadema 'kwishnei'

• Kila kimoja chatuhumu kusaliti maridhiano

**Januari Makamba na
falsafa ya umbo la maji**

Uk. 8



**Fidia Precision
kizungumkuti**

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kusan

Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI

MTN Airtel Vodacom Tigo Safaricom

**Changia uhai
wa Pambazuko**

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

Tahariri

Tanzania iondoe viza kwa Waafrika

NCHI nyingi za Afrika, sasa zinaanzisha utaratibu mpya wa kuruhusu wananchi wote kutoka nchi za bara hilo kuingia katika nchi moja kwenda nyingine bila kulalipia viza.

Imthibitika kuwa nchi za Afrika zinaweza kufanya biashara kubwa ya bidhaa – kutoka nchi moja hadi nyingine, kwa kuacha kutumia kizingiti cha kulipia viza, hivyo kuruhusu mwingiliano wa wafanyabiashara na hata bidhaa kirahisi.

Hatua hii imekuwa ikizinufaisha zaidi nchi za Ulaya, ambazo nyingi ziliachana na utaratibu wa wananchi wake kulipia viza wanapotoka ama kuingia katika nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU) na hata zisisokuwa wanachama.

Ni kutokana na kung'amua faida za mwingiliano kama huo, mataifa manne ya Afrika yametangaza kufuta malipo ya viza kwa Waafrika wanaoingia katika nchi hizo za Benin, Ushelisheli, Gambia na sasa Rwanda, ambayo Alhamisi ya wiki iliyopita ilitangaza kuondoa malipo ya viza kwa Mwafrika yoyote anayeingia nchini humo.

Akitangaza uamuzi huo, Rais wa Rwanda, Paul Kagame alisema “Mwafrika yeyote, anaweza kupanda ndege kuingia Rwanda wakati wowote anaotaka na hatalipa chochote kuingia nchini mwetu.”

Rais Kagame alieleza msimamo huo wa Rwanda wakati wa mkutano wa 23 wa Baraza la Utalii Duniani katika mji mkuu wa nchi hiyo, Kigali.

Kagame alibainisha kuwa licha

ya kukuza biashara kwa nchi za Afrika, inategemewa kuwa uamuzi huo utaongeza idadi ya watalii kutoka Afrika ambao wana shauku ya kutembelea Rwanda, lakini wanakwamishwa na mambo kadhaa, ikiwamo kiasi kikubwa cha fedha kulipia viza.

Mkuu huyo wa nchi anaamini kuwa asilimia 40 ya watalii wanaoingia Rwanda kutoka nchi za Afrika, wanaweza kuongezeka na kuwapiku watalii kutoka nje ya Afrika, ambao ndiyo wanatengeneza asilimia 60 ya watalii wote ndani ya nchi hiyo.

Mbali na nchi hizo nne za Afrika kuondoa viza, Rais wa Kenya William Ruto naye ameutangazia umma kwamba kuanzia Januari Mosi, 2024, nchi hiyo itaondoa malipo kwa Waafrika wanaoingia ndani ya nchi hiyo ya Afrika Mashariki.

Hakika sisi Pambazuko tunachukua fursa hii kupongeza wakuu wa nchi hizo tano kwa kufikia uamuzi wenye manufaa makubwa kwa usalama, uchumi na hata kugawana maarifa yanayopatikana Afrika.

Tunaamini kuwa Tanzania bado ina nafasi kubwa ya kufikia uamuzi kama huo ili kujihakikishia kukua kwa uchumi utakaochoweka na uimara wa mwingiliano wa wafanyabiashara na hata ongezeko la mapato kwa watalii wanaotoka ndani ya bara la Afrika.

Tanzania yenye vivutio lukuki vya utalii, inaweza kujihakikishia mapato zaidi kwa kuondoa malipo ya viza kwa Waafrika ili kuvutia watalii kutoka Afrika kuliko ilivyo sasa.

KAZI IENDELEE



Spika wa Bunge la Tanzania, Dkt. Tulia Ackson amechaguliwa kuwa raisi wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), katika kikao cha baraza la uongozi wa uoja huo kilichofanyika mjini Luanda, Angola – Oktoba 27, 2023. Tulia ndiye mwanamke wa kwanza wa Afrika kushika wadhifa huo. Hapa Spika Tulia akizungumza baada ya kutanagzwa mshindi. (Picha na IPU).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Ujenga wa Reli ya Kati (kutoka Dar es Salaam – Kigoma) ikiwa na kilomita 1254, ilijengwa kwa miaka miwili (1905-1907), wakati teknolojia ikiwa duni. Reli ya Tazara, yenye kilomita 1860, ilijengwa kwa miaka mitano (1968-73). Leo karne ya 21, reli kati ya Dar es Salaam – Morogoro, ikiwa na kilomita 300, inaendelea kujengwa kwa miaka saba hadi sasa. Hii ni aibu!
- Dkt. Chris Cyrilo.

Chalamila hebu kuwa siriazi basi!

Na Igo AI

TAI kavurugwa. Hajui sasa aendeleo kufuatilia na kuchambua maoni na matamano ya wabunge ya kunyongwa – hadi kufa, kwa watumishi wa serikali ambao ni majizi au aachane nao na kumsikiliza Gavana wa Dar es Salaam, Albert Chalamila?

Kwamba wakati wabunge wengi wanatokwa povu, wakizungumza kwa sauti za ukali na kuonesha kukasirika kwa kile wanachoeleza kuwa kuna “upigaji mkubwa” wa fedha za umma, gavana naye anakuja na zoezi la kuwafurusha machangudoa na kuvunja “ofisi zao.”

Tai kakabwa na msongo, je, adili na wabunge na matamano yao au akomae na gavana, kwa kumsaidia kuondoa machangudoa katika jimbo lake.

Hata hivyo, Tai anapata wazo, ngoja akomae na Chalamila, lakini siyo kwa kumsaidia eti kuwaondoa machangudoa na kuwatokomeza kabisa, bali kumshauri gavana awe siriazi kidogo na mambo makubwa ya kuondoa madhila kwa wanadalisalamu.

Tai akafunga safari. Akapiga mbawa zake hadi Ilala, pale ofisini kwa gavana ili amwambie ushauri wake “uso kwa macho.”

Holaaa! Gavana hayumo ofisini kwake na Tai akashauriwa na katibu muhtasi wake kuwa aache ujumbe au arejee siku inayofuata kwani boshi wa Dar es Salaam, yuko kwenye “oparesheni maalum.”

Operesheni maalum ya nini? Tai akahoji. Katibu muhtasi akasema; “kuondoa machangudoa Dar es Salaam.”

Tai akaaga na kuondoka. Akaiambia serikali ya kichwa chake kwamba hawezi kulala na jambo lake, lazima amuone Chalamila kokote aliko.

Tai akamsaka aliko Chalamila na bahati kamkuta mahali akiwa na timu ya wasaidizi wake – eti wakijiandaa kuanza bomoabomoa ya ofisi za machanguduo; akaomba kuzungumza naye.



Albert Chalamila, mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam

Na haya ndiyo mazungumzo ya Tai na Chalamila:

Tai: Hivi uchangukodo unaisha kwa kuvunja madanguro?

Chalamila: Hapana, lakini tunataka kuwaondoa kabisa, wanachafua jiji na kuharibu vijana wetu.

Tai: Hivi gavana, wewe unapambana na machangukodo au uchangukodo?

Chalamila: Vyote, lakini machangukodo hasa; kwani wewe unasemaje, sijakuelewa Tai.

Tai: Gavana, naomba kukushauri, hivi vita huviwezi, vimepiganwa tangu enzi za manabii, na machangukodo wakashinda, nawe wajiandalia aibu na anguko.

Chalamila: Usinitishe wewe Tai, mimi sijawahi kushindwa, wataondoka wote.

Tai: Sikutishi gavana, bali ushauri wangu kwako na serikali ni kuchukua falsafa ya mhariri mmoja – wa jina lako, akiitwa Kawogo, aliyeeleza kwamba katika hili zoezi, ni vyema tupambane na mifumo mbaya ya maisha inayozalisha uchangukodo.

Mifumo hiyo huleta ukosefu wa ajira kwa wahitimu, dhuluma ya haki, mgawanyo mbaya wa kijinsia katika pato la rasilimali, ukatili wa kijinsia, rushwa, matabaka katika elimu na maisha duni.

Baada ya ushauri huo, Tai akaona isiwe taabu, akaruka zake, maana gavana alionekana kupandwa hasira na akaanza kuzungumza kwa sauti ya juu.

Habari

Maridhiano CCM, Chadema 'kwishnei'

Na Tryuckia MFINANGA

MATAMANIO ya Watanzania kuona minyukano ya kisiasa isiyojenga staha, ustawi na kuaminiana baina ya vyama vya siasa, sasa yamezikwa.

Maridhiano ya vyama vikubwa viwili; chama tawala – Chama Cha Mapinduzi (CCM) na chama kiongozi cha upinzani, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) hayapo tena, baada ya wakuu wa vyama hivyo kutoaminiana.

Pambazuko linaelezwa kwamba pamoja na nia nzuri ya wenyeviti wa vyama hivyo, Rais Samia Suluhu Hassan (CCM) na Freeman Mbowe kutaka maridhiano, wasaidizi wao wamekuwa na hofu ya kufanikiwa.

Inaelezwa kuwa hofu hiyo inatokana na kila chama kushindwa kukubali moja kwa moja baadhi ya hoja na mapendekezo kila kimoja.

Akithibitisha kusimama kwa mazungumzo ya maridhiano hayo, Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, ameliambia Pambazuko wiki iliyopita kwamba CCM ndiyo chanzo cha kusimama kwa mazungumzo hayo.

Mnyika ambaye alisita kutamka kama yamevunjika moja kwa moja, alisema mazungumzo yamesimama tangu mwanzoni mwa Juni 2023.

“CCM ndio chanzo, hawataki mabadiliko yoyote ya maana ya kikatiba na kisheria, ili Tanzania iweze kuwa nchi inayosimamia misingi ya haki na kupatikana kwa maendelo ya uhakika kwa wananchi,” ameingiza Mnyika.

Anadai kwamba vitu vya haraka kwa sasa kwa taifa ni kuendelea na kukamilisha mchakato wa katiba mpya na pia kufanyika kwa marekebisho ya katiba



Rais Samia Suluhu Hassan

ya 1977 yenye kuwezesha uchaguzi huru na haki katika uchaguzi za mitaa 2024 na uchaguzi mkuu 2025.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu anasema kuwepo kwa mkwamo katika kuendelea na maridhiano hayo.

“Ni kweli kuna hali ya kupigania kidogo maridhiano, ila kwa kweli maridhiano haya hakuna kitu, yapo mambo CCM inayakataa, ambayo ni muhimu kwa ustawi wa Tanzania,” anasema Lissu.

Makamu wa Mwenyekiti wa CCM, Abdulrahman Kinana, anasema pamoja na kusimama kwa muda kwa maridhiano hayo, bado kuna nafasi ya kuendelea.

“Nina imani yataendelea hivi karibuni na mtasikia taarifa kutoka kwa viongozi wetu, hakuna kinachoweza kuharibika kabisa,” ameingiza Kinana.

Hata hivyo, mmoja wa wajumbe wa CCM katika maridhiano hayo, amesema Chadema wao ndiyo chanzo cha kusimama kwa maridhiano na kamwe siyo chama chake.

“Naomba nikwambie, Chadema ndiyo shida, wao wanataka kila walicholeta kikubalike na kianze kufanyiwa kazi haraka, halafu mapendekezo na mtazamo wetu, hawataki, hivi nani mkorofi hapo na nani asiyetaka maridhiano?” Amehoji na kuomba asitajwe jina kwa sasa kwani wapo wazungumzaji rasmi wa maridhiano hayo.

Wananchi wengi wamekuwa wakiamini kuwa maridhiano hayo yataendelea, lakini kuna kila dalili ya kuvunjika na huenda ikawa mwisho wake, hasa ikizingatiwa muda wa kuingia kwenye mchakato wa uchaguzi wa Mitaa na mkuu – mwaka 2025 unakaribia.

Fidia Precision bado kizungumkuti

Na Scovy MANASE

WAKATI leo unatimu mwaka mmoja tangu kutokea kwa ajali ya ndege ya Precision, bado baadhi ya manusura hawajapata stahiki zao zote, Pambazuko limeelezwa.

Tarehe ya leo mwaka jana, Novemba 6, ndege ya kampuni ya Precision Air ilipata ajali nje kidogo ya Uwanja wa Ndege wa Bukoba, huku abiria 19 wakifariki dunia, na 24 wakinusurika.

Baadhi ya manusura waliozungumza na Pambazuko mwishoni mwa wiki wamedai kwamba hawajapokea malipo yote stahiki, huku wahusika “wakionekana kupiga chenga.”

Manusura hao wameeleza kwamba tangu kulipwa kwa malipo ya fidia yaliyoitwa ya awali; dola za Marekani 5,000 (Sh. milioni 11.7 – wakati huo), kwa kila mmoja aliyenusurika, hawajapokea malipo mengine.

Pambazuko linataarifa kuwa kila familia ya abiria aliyefariki dunia ilipaswa kulipwa fidia ya awali ya dola 25, 000, sawa na Sh. milioni 58.5).

Baadhi ya manusura wameliambia Pambazuko kwamba wamekuwa wakizungushwa na kampuni, hasa ya mawakili na ushauri ambayo ilipewa kandarasi na Precision Air kusimamia fidia za manusura na familia za waliopoteza maisha.

Hata hivyo, Kampuni ya Precision Air, imeiliambia Pambazuko kuwa manusura wengi wameshalipwa stahiki zao, isipokuwa wachache wenye masuala yanayohitaji uamuzi wa mahakama na hata familia.

Akizungumza na gazeti la Pambazuko jana jijini Dar es Salaam, mmoja wa wakurugenzi wa Precision Air amesema; “wengi walionusurika wamelipwa, wapo wachache wanaosubiri mahakama kuamua, hasa masuala ya mirathi.” Amesema pia baadhi ya familia



“wamemalizana nao.”

Pambazuko limeona baadhi ya nyaraka zilizotumwa kwa manusura na familia za waliofariki dunia kwenye ajali ya ndege hiyo; ikiwemo barua ya Desemba 7, 2022 kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa Precision Air, Patrick Mwanri na hati ya malipo.

Mwanri katika barua yake anapokeza kuwa malipo hayo ya dola za Marekani 5,000 ni “kusaidia matumizi ya haraka ya matibabu na huduma zingine za maisha.”

Hati hiyo inaeleza kuwa mpokeaji anapewa malipo hayo kutoka kwa Precision Air pamoja na/au kampuni za bima zinazohusika kama malipo ya awali (Malipo ya Awali) na kwamba hati hiyo ya kupokea malipo itakuwa halali baada ya ‘Malipo ya Awali’ kufanyika.

Kwa mujibu wa kanuni ya 31 ya Kanuni za Mamlaka ya Anga Tanzania (Usafiri wa Anga) za mwaka 2008, Malipo ya Awali yanajumuisha malipo yatakayotolewa katika kiwango cha ziada kitakacholipwa na kampuni ya ndege pamoja na/au kampuni zake za bima kama fidia kutokana na majeraha na madhara aliyoyapata mhusika katika ajali ya ndege.

Mwanasheria Hamisi Kuleza ameliambia Pambazuko kuwa malipo hayo ya awali hayaathiri utetezi wa Precision Air au kampuni za bima zilizohusika ikiwa ni pamoja na matumizi ya pingamizi lolote linalowasilishwa na manusura ama familia na au taasisi yoyote.

Kampuni nyingi za uwakili zinasema abiria walionusurika walistahili fidia ya kati ya dola 75,000 hadi 120, 000. Na waliopoteza maisha wanastahili fidia ya dola 200,000 hadi 250,000 kutegemea na makubaliano.

Tafakuri

Makamba na falsafa ya umbo la maji

Na Hekima CHIUSE

WENGI wanaamini kwamba maji hayana umbo. Kwamba maji yapo tu kwa kuwa ni kimiminika ambacho hakina uwezo wa kusimama dede.

Hata hivyo, Wachina wamekuwa wakienda kinyume na mtazamo huo, kwani kwao kuna falsafa ya umbo la maji, ambayo ni maarufu zaidi katika kujenga uongozi, kufuatilia na kuchunguza mienendo ya watu wanaotaka kuwaongoza.

Kimsingi, hakuna kiongozi wa China ambaye anaibuka tu; kwa ngekuwa ama nguvu zingine ziwazo zozote, na kupata uongozi ndani ya taifa hilo lenye idadi kubwa ya watu. Inakadiliwa China ina watu wanaokaribia bilioni 1.426, ikiwa nyuma kidogo ya India ambayo sasa inatajwa kuwa na watu 1.428.

Kiongozi yoyote wa China “hupikwa” katika falsafa ya maji; kwa maana ya kufunzwa, kufundwa na kuelekezwa namna bora ya kuwa mwongoza njia kutoka kwa wakongwe wa siasa, tamaduni, uchumi na zaidi sana maisha ya taifa hilo lililomo ndani ya Bara la Asia.

Inaelezwa kwamba falsafa ya maji ambayo inaanzia katika China ya kale, inabeba maana kubwa kwamba maji yana umbo na umbo hilo hutegemea yako katika chombo gani.

Kwamba maji yanabeba umbo kulingana na chombo kinachohifadhi kimiminika hicho. Kihistoria, roho ya falsafa ya maji ina maana nyingi na kubwa za kiuongozi.

Kwamba lengo la Wachina kujenga falsafa ya maji, siyo kuchunguza lengo la fizikia yake, wala kuupa umma mtazamo wa kimetafizikia zaidi, la hasha, bali kukumbusha namna kiongozi wa watu anapaswa kuwa.

Ni kwa mantiki hiyo, kiongozi wa umma anapaswa kuwa msikivu, mnyenyekevu, mwenye kuthamini



January Makamba

miichango ya wenzake katika kuongoza na hata kupokea na kujali mawazo ya wale anaowaongoza.

Lakini kubwa zaidi kuonyesha njia kwa kukubali mitazamo chanya kutoka kwa wadau wengine ndani ya nchi. Awe kiongozi ambaye hapandishi mabega, wala kuwa na kinyongo kwa wengine.

Ni katika kuitazama falsafa ya maji kutoka China, namuona January Yusuf Makamba kuwa mmoja wa viongozi wachache katika Tanzania ambao wanaweza kuoanishwa na falsafa hiyo.

Uongozi wake, tangu awe waziri katika maeneo mbalimbali ndani ya serikali iliyokuwa ikiongozwa na Jakaya Kikwete, John Magufuli na sasa Rais Samia Suluhu Hassan, “hainui mabega,” hajiweki kimbelebele akijidai kuwa ni mjuzi wa maeneo mengi, hata kama aliwahi kuyaongoza.

Uongozi wa Makamba ni shirikishi, hata siku moja hajawahi kulalamikiwa kuburuza wenzake; kwenye changamoto ndogo ama kubwa, huita wadau na kushauriana nao na hatimaye kupatikana kwa muafaka.

Huyu ndiye kiongozi anayeonekana katika kioo cha falsafa ya maji ya China, kwa kusimamia wizara nyingi na kote amemudu na kuacha alama.

January Makamba anabeba tafsiri na taswira ya falsafa hiyo sasa.



Hoja Yangu

Afrika ikune vichwa kuondoa wakimbizi

Na Rashid MTAGALUKA

HIVI karibuni Rais wa Kamisheni ya Umoja wa Ulaya (EU), Ursula von der Leyen kutoka Finland, alialikwa na Waziri Mkuu wa Italia, Giorgia Meloni kutembelea kisiwa kidogo cha Lampedusa, ambacho ni kituo cha kwanza wanachofikia wakimbizi wanaotoka Afrika kwa kupita Tunisia.

Rais huyo wa Kamisheni ya Ulaya alifika na kuangalia wingi wa wakimbizi na kugundua kuwepo kwa ongezeko kubwa la watu “wanaokimbia” Afrika kwenda Ulaya.

Kwamba nchi wengi wanapenda kwenda Uingereza, ingawa nchi hiyo inaeleza kuzidiwa na wakimbizi kiasi cha kuanza mchakato wa kupunguza baadhi yao kuwahamishia nchi nyingine.

Mbali ya Afrika, zipo baadhi ya nchi kutoka Mashariki ya Kati na zile za Bara la Asia zinazozalisha kwa wingi wakimbizi wanaotokana na changamoto za kiusalama na kiuchumi kwa pamoja kama vile Pakistan.

Kwa Afghanistan, wakimbizi wake wanatokana na sababu za kiusalama na hasa tangu kuanza kwa utawala wa Taleban; wakiongoza kwa mhimili na itikadi za Uislamu.

Kwa ukanda wa Afrika, ukiondoa Eritrea, Ethiopia, Somalia, Sudan, DR Congo - kwenye changamoto za kiusalama, wakimbizi wake wanatokana na sababu za kiuchumi tu.

Nigeria, Ghana, Burkina Faso, Ivory Cost, Afrika ya Kati na Cameroon, sehemu kubwa ya kuwepo wakimbizi ni changamoto za kiuchumi. Watu wengi wa nchi hizo wamejawa fikra kwamba wakienda Ulaya wanaweza kuwa na maisha bora zaidi.

Binafsi mnyororo mrefu wa watu weusi

wanaokimbilia Ulaya kutafuta maisha - na baadhi tunawasikia wakizikufuru Neema za Mola wetu kwa kusema “heri kuzaliwa paka Ulaya, kuliko binadamu Tanzania, kama vile Ulaya hakuna masikini, inanisikitisha sana.

Aidha, kuna umuhimu mkubwa wa mawazo ya wanaumajumui wa Afrika, akiwemo Mwalimu Julius Nyerere, Kwame Nkrumah, Patrick Lumumba na wengineo waliokuwa wakipiga kelele Afrika kuwa taifa moja, kuanza kufanyiwa kazi!

Viongozi wetu wakubali kuacha uroho wa madaraka, yaani kila kiongozi katika hizi nchi, mwenye ndoto ya kuwa rais katika nchi yake, anawaza kama yeye ataweza kuja kuwa Rais wa Afrika, na mwingine anawaza na kujipanga kuwa waziri mkuu, je kukiwa na muungano, yeye ataweza kuwa waziri mkuu wa Afrika? haya ndiyo yanayotucheleweshwa kupiga hatua.

Kwanini viongozi wetu hawaigi kwa wenzetu walioendelea kama kile alichofanya rais wa kwanza wa Marekani, George Washington aliyeshawishi na kufanikiwa kuunganisha nchi 52 ambazo nyingine kama Florida ni kubwa kuliko Tanzania.

Mathalan, kijana akiona Rwanda maisha magumu anaweza kwenda Uganda, akiona Uganda hakufai, anaweza kwenda kuishi Senegal - kama ambavyo leo kijana wa Jimbo la Florida akiona maisha hayaelewielewi anakwenda jimbo jingine. Ni rahisi tu!

Kwa hiyo, katika mazingira ya namna hii najiuliza, lini viongozi wa nchi za Afrika watazinduka na kukaa pamoja kujadili mustakbali wa nchi kupunguza “kuzalisha” wakimbizi katika kuzi hao?

• *Wasiliana na mwandishi kwa simu: 0784438546 au Email; mtagaluka@gmail.com*

Habari**Wauguzi, wagonjwa wote wanateseka**

Na Mwandishi WETU

UNAPOONA muuguzi akimhudumia mgonjwa, unaweza kudhani ni mgonjwa pekee ndiye anakabili mateso ya maumivu, lakini hali siyo hivyo. Hata anayemuuguzi, yumo kwenye madhila.

Hali hiyo inathibitishwa na wauguzi wenyewe barani Afrika baada ya kueleza jinsi wanavyoteseka kisaikolojia katika kazi zao kwa kuwasababishia maumivu makubwa pengine kuliko hata wagonjwa.

Ripoti iliyotolewa hivi karibuni na Chama cha Wafanyakazi Duniani (Public Services International - PSI) inabainisha kuwa upungufu wa watumishi, ukosefu wa dawa na vifaa tiba pamoja na malipo duni, ni sababu zinazowatesa wauguzi na watumishi wa afya Afrika.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa karibia asilimia 60 ya wahudumu wa afya Afrika wameeleza kushuhudia wagonjwa wengi 'wakikata roho' mbele zao huku wakiwa wanasubiri kuhudumiwa.

Aidha, wauguzi wengine wameshuhudia jinsi wanavyoona wagonjwa wakiwa katika mateso makali ya maumivu, lakini hawapatiwi huduma zinazohitajika kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukosefu wa dawa na vifaa pamoja na uhaba wa watoa huduma.

Kushuhudia mtu akikata roho au akiteseka kwa maumivu kwa sababu tu ameshindwa kupatiwa huduma stahili, limeelezwa kuwa ni jambo linalowasababishia wauguzi wengi mateso kisaikolojia.

Isoyokuwa bahati, wauguzi na wahudumu wa afya wengi wanaangukia katika kundi hilo la watu wenye moyo ambao haupendi kuona binadamu akiteseka, lakini mazingira ya utendaji kazi yanawalazimisha kushuhudia hayo ambayo moyo yao haiyapendi.

Utafiti wa PSI umefanya uchunguzi wa uzoefu kutoka kwa wahudumu wa afya wapatao 2,200 kutoka nchi



Waziri wa Afya - Ummu Mwalimu (Picha kutoka mtandao)

12 barani Afrika na kubaini madhila hayoyanaywakumba wahudumu hao wa afya.

Wahudumu hao wa afya wameeleza kuwa ni jambo linalowasababisha msongo mkubwa wa mawazo kushuhudia mtu ambaye ulipaswa kuokoa maisha yake akifariki kutokana na sababu kuwa hakuna dawa, vifaa, wauguzi au madaktari wa kutosha kuwahudumia.

Katika utafiti huo takribani asilimia 60 ya wauguzi na madaktari barani Afrika wamebainisha kuwa wameshuhudia wagonjwa wengi wakifa wakati wanasubiri kuhudumiwa.

Baadhi ya nchi ambazo utafiti huo umefanyika ni Nigeria, Ghana, Afrika Kusini, Uganda, Malawi na Zimbabwe na kubaini kuwa upungufu wa watumishi ndio sababu kubwa inayosababisha wagonjwa wengi kufariki katika mazingira ambayo yanaweza kuzuilika.

Asilimia 71 ya waliohojiwa walikiri kuwa wanahudumia idadi ya wagonjwa mara mbili zaidi ya idadi ambayo imewekwa kitaaluma. Wanalazimika kufanya hivyo kutokana na upungufu wa washudumu wa afya katika maeneo mengi.

Zaidi ya theluthi mbili ya wauguzi waliohojiwa walibainisha kuwa wanalazimika kutimiza majukumu yao wakiwa na vifaa vichache na duni wakati asilimia 80 kati yao wakilalamika kufanyishwa kazi kwa muda mrefu sana zaidi ya ule waliokubaliana katika mikataba yao ya kazi.

Ni wakati wa Takukuru nao kudhibitiwa

Na Rashid Mtagaluka

WAZIRI wa Nchi ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene amekaririwa akisema kuwa, kazi kuu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) siyo kupambana na rushwa, bali ni kuzuia kabla haijatokea.

Simbachawene alitoa kauli hiyo Oktoba 7, 2023 mjini Moshi mkoani Kilimanjaro wakati wa hafla fupi ya kufunga mafunzo ya awali kwa maofisa 370 wa taasisi hiyo yaliyofanyika katika Chuo cha Polisi (CCP).

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, malengo ya serikali ni kuhakikisha wahitimu hao wanakwenda kuzuia zaidi mianya ya rushwa na ikishindikana, basi wakapambane nayo.

Kauli hii ya Simbachawene ni nzuri sana, kwa sababu inamuonesha mhitimu nini jukumu lake la msingi analopaswa kuitekeleza.

Aidha, ni kauli inayokumbusha maneno ya Rais Samia Suluhu Hassan katika moja ya hotuba zake, alizozitua ziarani wilayani Kilwa, Lindi Septemba, 2023.

Rais Samia aliwataka watendaji wa Takukuru kujikita kwenye kuzuia rushwa ili fedha “zinazoshushwa chini” kwa ajili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi, zitumike vizuri bila kuingia kwenye mifuko ya wajanja wachache.

Hata hivyo, inasikitisha kila kukicha tunasikia kukithiri kwa vitendo vya rushwa katika sekta na maeneo anuwai hapa nchini.

Ni wazi kwamba ukithiri kwa vitendo vya rushwa katika taasisi za umma hapa nchini kunajulikana kwa wananchi wengi, inakuwaje maofisa waliosomea darasani namna ya kunusa dhambi hii wasiwe na taarifa?

Kwa mfanano, uwepo wa taarifa za



Mkurugenzi Mkuu Takukuru - Salum Hamduni

udanganyifu, wizi na ufisadi wa fedha za umma, baadhi ya vigogo kumiliki kampuni za ujenzi na hivyo ‘kujipasia’ zabuni wenyewe kupitia kwa marafiki zao, ni kielelezo cha taasisi hiyo kushindwa kusaidia nchi.

Ni kutokana na kupwaya kwa Takukuru, natamani kuona siku moja serikali inapeleka muswada bungeni kuwepo ‘lichombo’ maalum kuchunguza Takukuru.

Maana uwepo wa Takukuru, wengi waliamini sasa nchi yetu itaepukana na changamoto za uwepo wa watendaji katika taasisi za umma na binafsi wenye kujihusisha, kuomba na kupokea rushwa.

Lakini, inavyoonekana watu wameanza kukata tamaa, ni kama vile Watanzania walivyoshinda juani kwenye misururu mirefu ya kujiandikisha kwenye usajili wa kielektroniki wa namba za simu wakiaminishwa na mamlaka kuwa sasa utapeli, matusi, wazee wa “Tuma kwenye namba hii” itakuwa mwisho, ilihali mpaka leo wezi hao wanaendelea kunepena kwa wizi kupitia simu za mkononi.

Ebu sasa tusaidie na kiongozi wake, Rais Samia kutokomeza hili dubwana la rushwa, la siyvo tushauri hii taasisi ivunjwe au iundwe nyingine ya kuichunguza Takukuru ili nayo izeze kudhibitiwa katika kukomesha rushwa Tanzania.

Mwandishi anapatikana kwa simu 0784 438546 au Email: mtagaluka@gmail.com

Mtazamo**Tume ya Uchaguzi Z'Bar ijitafakari**

Na Jabir IDRISSE,
Zanzibar

WANANCHI wa Jimbo la Mtambwe, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, walipiga kura Jumamosi iliyopita kumchagua mjumbe mpya wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Uchaguzi huo ulifanyika kuziba nafasi iliyokuwa wazi kufuatia kifo cha Habibu Mohamed aliyetangazwa kuwa mshindi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Kwa mujibu wa tangazo la matokeo lililosomwa usiku huo na msimamizi wa uchaguzi huo, Othman Khamis Othman, wananchi hao walimchagua Dkt. Mohammed Ali Suleiman wa Chama cha ACT-Wazalendo aliyepata kura 2449.

Msimamizi Othman alitangaza kuwa Dkt. Mohammed, mtaalamu wa kada ya ununuzi wa umma na mifumo ya mawasiliano ya kiteknolojia, alimshinda Hamad Khamis Hamad aliyegombea kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), akiwa amepata kura 1531.

Wagombea walioshiriki uchaguzi huo walikuwa ni Said Nassor Hemed wa Chama cha Wananchi (CUF), aliyepata kura 43 na Mohamed Masoud wa Chauma ambaye alipata kura 22.

Hakika wananchi wa jimbo hili lililoko kando ya Bandari ya Wete, Pemba, wametumia haki yao ya kikatiba ya kuchagua.

Lakini kwa kupima namna utekelezaji huo wa haki ya kuchagua ulivyofanyika, siyo aibu wala fedheha kutamka kuwa uchaguzi huo umethibitisha - kwa mara nyingine, Serikali ya CCM haijawa tayari kusimamia haki za msingi za wananchi kwa msingi wa haki na kufuata sheria na taratibu ambazo yenyewe imeziandaa na zikatungwa.

Kwa mfano, unahesabu vipi kura bila ya kuruhusu vishina vya vitabu vya karatasi za kura kuhakikiwa kwanza? Kwa kukwepesha vishina vya vitabu vya



Dkt. Mohammed

karatasi za kura kuhakikiwa, unapata picha kuwa hakukuwa na uchaguzi wa haki na ulio huru. Kulikuwa na udanganyifu.

Ni nani ataamini kuwa kura zillotangazwa kwa halali ndio hizo zilizopigwa na wananchi? Na kama zote ni kura halali, kulikuwa na haja gani ya kuwatoa mawakala vituoni wakati wa maandalizi ya kuhesabu kura?

Na ikatokea kuwa mawakala waliotolewa kwa njama wote wawe ni wa Chama cha ACT-Wazalendo pekee? Na ukizingatia ukweli kuwa chama hiki ndio chenye ushindani kwa CCM?

Hapana shaka wasimamizi wa uchaguzi kwenye vituo, kwa maelekezo mahsusi, waliamua kuwawekea mkwara mawakala wa upinzani kwa madhumuni ya kufanikisha mpango wa kukisaidia chama tawala kilichokuwa kikitaka lazima kitwae kiti cha uwakilishi hata kama hakijawahi kufanya hivyo kupitia uchaguzi huru na wa haki tangu mwaka 1995.

Mgombea Dkt. Mohammed wa ACT, ambaye sasa ni Mwakilishi, alikabidhiwa kura tele na wananchi waliokuwa wamekatiwa zaidi ya kura moja, na mgombea akazionesha kwa vyombo vya habari.

Inashangaza kwamba hizi ni kura

Tume ya Uchaguzi Z'Bar ijitafakari

Inatoka Uk. 12

halali, lakini kwa kuwa ziligawiwa kwa wapigakura ambao walishakatiwa kura mojamoja, zinakuwaje zitumike tena wakati sheria inaeleza mfumo wa “mtu mmoja kura moja?”

Na kama uchaguzi huo mdogo wa Mtambwe ulifikia hatua ya kushuhudia msimamizi msaidizi akingawia mpigakura mmoja zaidi ya kura moja, anaweza kueleza ni nani aliyempa mafunzo au maelekezo ya kufanya hivyo wakati anajua sheria ya uchaguzi na kanuni zake, inashurutisha kila mpigakura atapaswa kupewa kura moja akifika mbele ya msimamizi msaidizi wa kituo?

Je, Tume ya Uchaguzi inaweza ikatoka maelezo ya maana kutetea utaratibu huu uliotumiwa na watendaji walioajiriwa kwa ajili ya kusimamia uchaguzi huu wa jimboni Mtambwe?

Haiwezekani wasimamizi na wasaidizi wao vituoni watumie utaratibu wa kumgawia mpigakura zaidi ya kura moja kwa uamuzi wao binafsi.

Wapo wananchi watakuwa tayari kueleza namna walivyotendewa na wasimamizi wa uchaguzi huu.

Kasoro hizi za usimamizi wa sheria na kanuni za uchaguzi, ndizo zinajenga uhalali wa hoja kuwa lipo tatizo kubwa kwenye Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar katika namna inavyoendesha majukumu yake ikiwemo usimamizi wa uchaguzi.

Inapotokea kuwepo watendaji katika nyanja ya usimamizi wa uchaguzi vituoni, maana yake sekretarieti ya tume hiyo ndiyo inayohusika kwa kuwa ndio yenye dhamana ya kuajiri watendaji kwa ajili ya kusimamia shughuli ya uchaguzi.

Moja ya maeneo ambayo yanalalamikiwa kuhusu utendaji adilifu wa tume hii sekretarieti. Imekuwa mdomoni kila unapofika uchaguzi kwa kuwa ndio injini ya utekelezaji wa majukumu ya tume.

Sekretarieti hii ndiyo yenye dhamana ya kuajiri, kununua, kuendesha mafunzo kwa watendaji wa tume na kulinda na kutunza mali zake. Ndio inayopanga mchapishaji wa karatasi za kura pamoja na vifaa vingine mbalimbali vya uchaguzi.

Kama haitendi kazi zote hizo kwa uadilifu na weledi licha ya ukweli kuwa inatarajiwa kujumuisha watendaji wenye utaalamu wa fani anuai, matendo yanayoyoshuhudiwa wakati wa uchaguzi, ndio ushahidi usiokuwa shaka wa kushindwa kwake majukumu.

Sekretarieti kwa kuwa ndio moyo wa utendaji wa tume, inatakiwa kuvunjwa na hapa ndipo yale mapendekezo ya kupatikana kwa Tume Huru ya Uchaguzi yanapokuwa na nguvu.

Wala isionekane kuwa marekebisho yanayokusudiwa kuwa yafanyike yanalenga kuiondolea CCM manufaa inayopata, hayo ni maslahi yake, ambayo hayana maana yoyote mbele ya maslahi mapana ya umma.

Kila hatua ya serikali kutekeleza majukumu yake, izingatiwe kuwa lengo kuu ni kuleta matunda yenye maslahi kwa wananchi ambao ndio wenye mamlaka ambayo ni wao huyatoa kwa watu wachache kwa minajil ya kuongoza kiuwakilishi wa wananchi wote katika nchi.

Hakuna namna CCM na viongozi wake wanaweza kuendelea kukwepa marekebisho yanayotakiwa na wananchi kwa mifumo ya uendeshaji wa uchaguzi kwa sababu uchaguzi ni haki yao na ndio njia pekee ya nchi kupata uongozi kwa njia ya kidemokrasia kwa amani kamili.

Kwa vile wenyewe watawala wanaaminisha kwa maneno yao kutaka siasa za maridhiano, siyo vyema nchi kuendelea kuendesha jukumu hili kwa njia za kubahatisha kama vile watu katika familia wanavyopiga ramli ili kumuamla mgonjwa wao tiba yake.

Habari

Jaji Warioba afunda watoto Moga

Na Scovya MANASE

JUMAMOSI ya Oktoba 14, mwaka huu, itabaki kuwa kumbukumbu muhimu kwa walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi Moga, baada ya kupata wasaa wa kuzungumza na Jaji Joseph Sinde Warioba.

Pamoja kwamba siku hiyo ni mahsusi kwa kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere – watu wengi hupumzika, wanafunzi wa Moga Schools waliamua kumtembelea Jaji warioba nyumbani kwake, Dar es Salaam katika kuadhimisha siku hiyo, kinyume na mazoea.

Jaji Warioba, ambaye pia aliwahi kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, aliwaasa wanafunzi hao kuiga mema aliyofanya na kuyaamini Mwalimu Nyerere. Nyerere ndiye rais wa kwanza wa Tanganyika na baadaye Tanzania.

Akieleza wasifu wa Mwalimu Nyerere, Jaji walioba alisema kiongozi huyo alikuwa muumini mkubwa wa kufanya kazi kwa bidii, kwa weledi na bila kuonea mtu.

Kwamba Mwalimu Nyerere alikuwa mpenda haki na kila mara alifanya majukumu yake na kuyatekeleza kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania na sheria zingine.

“Mwalimu Nyerere hakuwahi kuwa



Jaji Warioba akiwa na watoto

mbinafsi, hakuwa mbadhirifu hata kidogo na alitenda kwa wema bila kuonea mtu,” aliongeza Warioba.

Kutokana na kuainisha baadhi ya sifa za Mwalimu Nyerere, Jaji Warioba akawaasa wanafunzi wa Moga na vijana wa Tanzania kwa ujumla wao, kuiga maisha ya muasisi huyo wa Tanzania.

Wanafunzi wa Moga Schools, licha ya kuzugumza na Jaji warioba, pia walimkabidhi tuzo ya mwanasiasa mahiri na mpenda haki.

Pia wanafunzi hao walitumia siku hiyo maarufu – Nyerere Day, kusafisha mazingira katika maeneo yanayozunguka nyumba ya Jaji Warioba na pia walipanda miti ikiwa ni kuweka kumbukumbu zaidi.



Jaji Warioba akiwa na watoto



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Uchambuzi

Nini kinachofichwa kupitia ripoti za CAG

Na Mwandishi WETU

MTU ambaye anatua Tanzania leo, kisha akapata wasaa wa kusikiliza wabunge wakitoa michango yao baada ya kusomewa ripoti za kamati za kudumu za bunge zinazohusika na uhibitaji wa fedha za umma, anaweza kudhani kuwa nchi hiyo ina bunge kali ambalo linaifanya kazi ya kuisimamia serikali kwa ufanisi wa hali ya juu.

Kwa kiasi kikubwa ripoti za kamati hizo – Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) – zinachambua ripoti ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Ripoti za CAG ziliwasilishwa Bungeni mwezi Aprili mwaka huu na hivi sasa ndipo wabunge wanapata nafasi ya kujadili ripoti hizo ambazo zimechambuliwa kupitia ripoti za kamati.

Unaweza kuona au kudhani kuwa bunge limechelewa sana kujadili ripoti hizo, lakini hali iko hivyo kutokana na mtiririko wa shughuli za Bunge.

Ukiwasikiliza wabunge unaweza kudhani kuwa bunge linaisimamia serikali kwa ukali kutokana na ukali ambao wabunge wanaonesha wanapojadili ripoti hizo.

Wabunge wanaonekana kusikitishwa sana na kile wanachokiita kuwa ni wizi mkubwa wa fedha za serikali ulioibuliwa na CAG kupitia ripoti zake za ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2021/22.

Wabunge wengi wamezungumza kwa sauti kali zenye kubeba uchungu wa hali ya juu kutokana na wizi huo ulioibuliwa na CAG kiasi cha kufikia hatua ya kupendekeza kuwa watumishi wa umma waliohusika na ubadhirifu huo mkubwa wa fedha wakatwe mikono.

Lakini wapo wabunge ambao wamekwenda mbali mno kwa kupendekeza kuwa watu waliohusika



Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu -Charles Kichere

na ubadhirifu huo wa fedha za umma, wanyongwe.

Inashangaza kuwa wakati huu wabunge wanaonekana kuwa wakali kwa ubadhirifu ulioelezwa kwenye ripoti za CAG - wakati ripoti hizo za CAG hutolewa kila mwaka zikionesha mambo yaleyale; ya wizi wa fedha za umma.

Hakuna mwaka ambao ripoti za CAG zimetolewa zikaonesha kuwa matumizi ya fedha za umma yako safi. Kila mwaka, CAG amekuwa akionesha udhaifu mkubwa katika kutunza hesabu na kuonesha viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kiwango kikubwa.

Lakini, inaonekana wabunge wameiona ripoti hii tu!

Ni wabunge hawahawa ambao kila mara tumekuwa tukiwasikia wakitoa hongera na pongezi kwa serikali, na hasa kwa rais anayekuwa madarakani.

Ileweke kuwa hawa wabunge wamekuwa “wakimwagiwa” mabilioni ya shilingi katika majimbo yao, fedha ambazo zinataraajiwa kutekeleza miradi kadhaa ya maendeleo na kuimarisha huduma za jamii.

Katika ziara ya viongozi wa juu serikalini katika maeneo mbalimbali, kila wanapopewa nafasi kuzungumza katika mikutano, wabunge wamekuwa wakimshukuru rais kwa kuwapatia fedha nyingi kwa ajili ya huduma za jamii na miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Ni nadra sana kusikia mbunge

Nini kinachofichwa kupitia ripoti za CAG

Inatoka Uk. 16

akilalamikia matumizi mabaya ya fedha hizo za umma, sasa inakuwaje leo waibuke na kuanza kuunga mkono ripoti za CAG zinazoonedha ubadhirifu mkubwa?

Jambo ambalo kimsingi ni tofauti na kile ambacho wamekuwa wakikisema wanaposhukuru rais kwa kuwaletea mabilioni ya fedha zilizotumika vizuri sana katika maeneo yao?

Inashangaza kuwa wabunge “wanakuja juu” wakati huu kuhusu kile kilichoelezwa na CAG katika ripoti yake wakati kiuhalisia kinachoelezwa na CAG katika ripoti hizo hauwezi kukiita kuwa ni wizi wa fedha za umma.

Kimsingi, anachoonyesha CAG ni upungufu katika utunzaji wa hesabu unaotokana na kutotekeleza matakwa ya kiuhasibu kwa wanaohusika.

Kinachoibuliwa na CAG ni hoja za kijasibu na nyingi ya hoja hizo hujibiwa na kufungwa baada ya wahusika kurekebisha kasoro zilizoonyeshwa.

Zipo hoja ambazo zinaonesha wasiwasi wa matumizi mabaya ya fedha kwa sababu tu hakuna nyaraka za kuthibitisha matumizi hayo, lakini nyaraka hizo zinapopatikana na kufikishwa kwa mkaguzi, hoja kama hiyo hufa.

Ni kweli zipo hoja chache ambazo hazijibiwi kikamilifu na hoja kama hizo ndizo ambazo hasa zinazotakiwa kuangaliwa kwa jicho la ubadhirifu au wizi.

Kinachopaswa kufanyika baada ya hoja hizo kushindwa kujibiwa au kujibiwa kwa majibu yasiyorodhisha, ni uchunguzi ili kukusanya ushahidi wa kuthibitisha ubadhirifu na kisha wahusika kuchukuliwa hatua zinazostahili, ikiwemo za kinidhani na kisheria kama vile kufukuzwa kazi au kushitakiwa mahakamani.

Kuna jambo jingine linaongeza utata kwenye suala hili. CAG huyohuyo katika ripoti yake ambayo imeibua hisia za



Spika wa Bunge - Tulia Ackson

wabunge, ameeleza kuwa ni halmashauri 13 tu ndizo zimepata hati zenye mashaka kwenye ukaguzi uliofanyika huku halmashauri zaidi ya 170 zikipata hati safi.

Sasa kama halmashauri nyingi nchini zina hati safi kwa mujibu wa CAG, huo wizi mkubwa unaopigwa kelele na wabunge upo wapi?

Hali kama hii ya taasisi nyingi kupata hati safi ipo pia kwa taasisi za serikali kuu. Sasa kama taasisi nyingi za serikali zina hati safi, huu wizi unaolalamikiwa na wabunge umetokea wapi au umetokeaje?

Hoja hizi hazimaanishi kutetea wizi, la hasha. Inavyoonekana kuna namna ambayo inafanyika ili kuficha hali halisi kuhusiana na matumizi ya fedha za umma.

Haiwezekani wabunge walalamikie wizi mkubwa wakati CAG akiwa ametoa hati safi za ukaguzi kwa taasisi nyingi.

Kwa upande mwingine, serikali imejibu baadhi ya hoja zilizoibuliwa na wabunge wakati wakichangia ripoti hizo na kuonesha baadhi ya watu waliochukuliwa hatua baada ya ripoti ya CAG kuonesha ubadhirifu unapohisiwa kutokea katika maeneo yao.

Wakiwa majimboni wabunge wanapongeza serikali kutoa fedha nyingi za miradi na huduma, wakija bungeni wanalalamikia wizi na ubadhirifu mkubwa.

Kuna jambo halijaa sawa.

Lesotho

Usalama Lesotho bado hakijaeleweka

Na Mwandishi MAALUM

HALI ya salama ndani ya Lesotho bado hufutwa. Kuvutana viongozi wakuu; ukoo wa kifalme, wakuu wa mila, waziri mkuu na timu yake kunaashiria kulipuka kwa mgogoro mkubwa endapo hautadhibitiwa mapema.

Kutokana na hali hiyo, Umoja wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) umewaagiza Jakaya Kikwete, rais mstaafu wa Tanzania na Rais wa Zambia, Haikande Hichilema kuhakikisha wanakutanisha viongozi hao wa Lesotho ili kunusuru machafuko.

Alhamisi ya wiki iliyopita, Kikwete aliungana na Rais Hichilema kukutana na viongozi mbalimbali wa Ufalme wa Lesotho kama sehemu ya mchakato wa kutafuta suluhu ya mgogoro wa kisiasa na kiusalama uliopo Lesotho.

Viongozi hao wawili waliwasili Maseru, mji mkuu wa nchi hiyo na kuzungumza na viongozi hao ikiwa ni kutekeleza maagizo ya wakuu wa nchi na serikali wa SADC kusaidea nchi hiyo kukamilisha mchakato wa kutafuta amani ya kudumu katika Ufalme huo ambao haujawahi kupata amani ya kudumu tangu ulipopata uhuru hadi sasa.

Rais Hichilema aliongoza ujumbe huo akiwa Mwenyekiti wa Ogani ya Utatu ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Umoja wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC Organ Troika).

Rais Kikwete aliambatana naye kwa nafasi yake ya Mwenyekiti wa Jopo la Wazee la SADC (POE) ambapo ndiye aliyekabidhiwa jukumu la kuongoza timu ya usuluhishi wa mgogoro huo wa Lesotho.

Pamoja na mambo mengine, viongozi hao walipata fursa ya kuonana na Mfalme Letsie III wa Lesotho, Waziri Mkuu wa Nchi hiyo, Samuel Matekane pamoja na viongozi wa vyama vya upinzani nchini



Mfalme Letsie III

humu.

Katika Mkutano wao na Matekane, SADC ilipokea taarifa ya Serikali ya Ufalme huo katika kutekeleza mchakato wa kupitisha bungeni muswada wa mabadiliko ya kudumu ya baadhi ya sheria unaoaminika na wengi kuwa ndiyo muarobaini wa kudumu wa changamoto mbalimbali zinazoikabili nchi hiyo.

Waziri mkuu huyo alielezea nia ya dhati ya serikali yake kusimamia na kuhakikisha kuwa muswada huo unapitishwa kama inavyotarajiwa na wengi.

Aidha, katika kikao na viongozi wa umoja wa upinzani walipata fursa ya kusikiliza na kueleza mtazamo wao ambao wanaamini unaweza kumaliza mgogoro wa siasa na usalama katika taifa hilo lenye watu wanaokadiriwa kufikia milioni 2.5.

Kwa upande wao, Rais Hichilema na Kikwete walitumia fursa ya kukutana na viongozi hao kusisitiza umuhimu wa pande zote zinazohusika katika kutafuta suluhu ya kudumu nchini humo, kutanguliza maslahi mapana ya Lesotho ili kukamilisha mchakato huo uliofikia katika hatua nzuri ya majadiliano.

Waziri Mkuu Matekane, tajiri mkubwa wa madini, baada ya kuingia madarakani mwaka jana, aliapa kumaliza ufisadi, lakini anadai hadi leo anakwamishwa na Mfalme Letsie III.



Ahukumiwa kunyongwa kwa kumuua 'hawara' wa mume

Gazeti la Pambazuko kuanzia wiki hii linakuletea mfululizo wa baadhi ya kesi zilizowahi kusisikua umma kutokana na matukio ya kuogofya. Tunaanza na shauri la Asha Mkwizu aliyehukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji ya mwanamke aliyedai kuwa hawara wa mume wake. Endelea...

NOVEMBA 19, 1983 mwanamke mmoja, akiitwa Mwanahamisi Happiness Senzota alikwenda Kituo cha Polisi cha Salender Bridge, Dar es Salaam.

Alipofika kituoni alikutana na askari wa upelelezi, Haruna Masumai na kueleza shida ya kufika kituoni hapo, baadaye alianza kuchukuliwa maelezo yake ambayo yalikuwa ni malalamiko kwamba mwanamke mmoja, aliyejulikana kwa jina la Asha Mkwizu ametishia kumdhuru.

Mpelelezi huyo alifanya mawasiliano na mtuhumiwa na siku mbili baadaye, yaani Novemba 21; wote wawili - mlalamikaji Happiness Senzota na mtuhumiwa Asha Mkwizu walifika kituoni hapo kama walivyoelekezwa na askari huyo wa upelelezi.

Kulingana na maelezo ya awali ya Asha, ilielezwa kwamba Happiness alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mume wa Asha Mkwizu aliyetajwa kwa jina la Dkt. Hauli. Baada ya kuchukua maelezo yao aliwaambia waondoke na kurejea siku inayofuata, yaani Novemba 22.

Kwa mujibu wa kijana wa kazi wa Asha Mkwizu, aliyejulikana kwa jina la Musa James, alidai kwamba mnamo tarehe hiyo ya 22 Novemba, 1983, bosi wake, Asha Mkwizu alimtuma kwenda kununua mkaa, baada ya kuwa ameandaa chai. Baada ya kurejea, Musa alidai kwamba alikwenda kumwagilia maji katika bustani, ambapo alidai pia kuona shimo la urefu wa kama futi tatu kwenda na



Asha Mkwizu akiwa amefunika uso baada ya kutoka kusikiliza hukumu yake.

chini upana wa futi tatu na nusu hapo bustanini.

Musa alidai kwamba alitakiwa na Asha kwenda kununua mkaa maeneo ya Kariakoo na alielezwa kwamba asirudi nyumbani kabla ya saa sita mchana.

Inadaiwa kwamba, baada ya Asha Mkwizu kutoa maelekezo hayo kwa kijana wake, aliondoka kwenda kituo cha Polisi cha Salender Bridge kama walivyotakiwa na askari wa upelelezi wa kituo hicho.

Asha Mkwizu alipofika hapo kituoni alimkuta Happiness na ndipo walipoongozana kuingia ndani kukutana na askari wa upelelezi. Walimkuta na kuzungumza.

Hata hivyo, askari huyo aliwaambia kwamba asingeweza kusikiliza shauri lao kwa sababu Dkt. Hauli hayupo nchini kwa hiyo wasubiri mpaka hapo atakaporudi, ndipo wazungumzie shauri lao na kupatiwa muafaka.

Askari huyo wa upelelezi aliwasihi wasije wakadhuriana wakati wanamsubiri Dkt. Hauli. Baada ya kuwaonya Happiness ndiye aliyekuwa wa kwanza kuondoka na

Kesi zilizosisimua

Ahukumiwa kunyongwa kwa kumuua 'hawara' wa mume

Inatoka Uk. 19

baada ya dakika 10 hivi, Asha Mkwizu naye akaondoka. Huo ndio ulikuwa mwisho wa Mwanahamisi Happiness Senzota kuonekana akiwa hai.

Kwa mujibu wa kijana wa kazi wa Asha Mkwizu, alidai kwamba alirudi kutoka Kariakoo kununua mkaa na alipofika nyumbani alimkuta mdogo wake Dkt. Hauli aitwae Robson Hauli akiwa hapo nyumbani. Pia alimkuta bosi wake.

Asha alimwambia Musa aandae ndizi kwa ajili ya watoto, lakini Musa alishangaa kuona damu nyingi na akauliza zimetoka wapi?

Asha alimwambia Musa kwamba amejumiza na alimtaka asafishe damu pale sebuleni na kule bafuni pia ambapo damu ilikuwa imeanza kuganda ukutani.

Hata hivyo, inadaiwa kuwa Novemba 24, 1983, Asha alimweleza Musa - "Nimemmaliza adui yangu."

Musa alipomuuliza ni nani huyo adui yake aliyemmaliza, Asha alimjibu kuwa ni Happiness Senzota. Asha aliendelea kumweleza Musa kwamba amemua Happiness na kumzika katika eneo la hapo nyumbani, lakini alikataa kumuonesha Musa mahali alipouzika mwili huo.

Novemba 27, 1983, Musa alikwenda kuripoti jambo lile Polisi, ikiwa ni kinyume na onyo la bosi wake, kwamba atunze siri hiyo na asije akamweleza mtu yeyote kuhusu jambo hilo.

Baada ya Musa kuripoti Polisi, Asha alikamatwa na baada ya kuhojiwa na kufanyika kwa uchunguzi, Polisi walibaini ulipozikwa mwili wa Happiness.

Polisi waliufukua mwili huo na baada ya uchunguzi wa awali ilitibitishwa kwamba mwili ule ulikuwa ni wa Mwanahamisi Happiness Senzota.

Uchunguzi zaidi ulionesha kwamba ule mwili ulikuwa na majeraha matatu; jeraha moja katika mkono wa kushoto, na majeraha mawili yalikutwa kichwani - moja likiwa kubwa kwa upana wa sentimetra tano, likiwa na kina kirefu kiasi cha kufumua ubongo. Hili jeraha ndilo lililoelezwa na daktari aliyefanya uchunguzi wa sababu za kifo hicho cha Happiness Senzota.

Novemba 29, 1983- askari mpelelezi wa shauri hilo, Alfred Gewe, alimhoji mtuhumiwa na baadaye mlinzi wa amani naye alimhoji mtuhumiwa huyo, ambapo maelezo hayo yalitumika kama ushahidi pale mahakamani.

Katika kesi hii ni ya mwaka 1983 - Asha Mkwizu Hauli, alishitakiwa na Jamhuri kwa kosa la kumuua kwa kukusudia Mwanahamisi Happiness Senzota Novemba 22, 1983 nyumbani kwake Mtaa wa Lugalo, Upanga. Dar es Salaam.

Kosa hilo la kuuwa kwa kukusudia (Murder) limeainishwa kwenye kanuni ya adhabu (Penal Code) kifungu cha 196.

Kesi ilisikilizwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania jijini Dar es Salaam na Jaji Anthony Bahati akisaidiwa na Wazee wa Baraza waliojulikana kwa majina ya Bi. Mwasabuli Ali na mwenzie, Mzee Kikoti.

Upande wa mashtaka katika kesi hii waliita jumla ya mashahidi 14 na

Itaendelea Wiki Ijaye

KUNRADHI

Tumelazimika kusimamisha mwendelezo wa riwaya ya Tetemeko la Ndumba, iliyokuwa ikichapishwa kwenye ukurasa huu. Hii inatokana na sababu nje ya uwezo wetu. Tunaomba radhi kwa usumbufu huo.

- Mhariri

Neema kubwa yanukia kwa Majiha

Na Nestory NESTORY

NYOTA ya bondia Mtanzania, Fadhili Majiha, imeendelea kung'ara baada ya kumchakaza ulingoni, Bongani Mahlangu kutoka Afrika Kusini wiki iliyopita.

Katika pambano la raundi 10 – uzito wa Super Bantam, lililofanyika Ukumbi wa PTA, Dar es Salaam, Majiha alionesha namna ngumi za “hesebu na wepesi” zinavyochezwa na kuwa burudani murua kwa watazamaji.

Ushindi huo umemfanya Majiha kuwa bingwa wa kwanza wa mkanda wa WBC –Afrika.

Tovuti maarufu inayofuatilia mabondia duniani; Boxrec, inaonesha kuwa Majiha ndiye bondia nambari wani Tanzania na Afrika na kwamba ni nambari 34 duniani kwa ubora katika uzito wa Bantam; kilo 55 hadi 61.

Kufuatia kuwa na rekodi nzuri ya kuchakaza wapinzani wake, sasa Majiha

anaweza kuvuka mabara na kuwekeza nguvu zake kupigana na mabondia wa dunia ya kwanza – hasa kutoka Marekani.

Ikiwa atafanikiwa – kwa msaada wa mapromota makini, jina la Majiha na Tanzania vitajaa sifa na heshima kuu katika medani ya masumbwi, hivyo kuwa chanzo kikuu cha utajiri na neema zingine kwake na kwa nchi.

Kimsingi, mchezo anaonesha Majiha anapokuwa ulingoni, ni dhahiri kwamba kiwango chake kwa sasa kinavuka mipaka, isipokuwa anatakiwa kuongeza pumzi ya kuhimili raundi nyingi zaidi, na hasa kufikia 12.

Ikiwa atakuwa na pumzi ileile anayoanza nayo, kama alivyoonesha kwenye mchezo wake dhidi ya Bongani wiki iliyopita, basi Tanzania itakuwa na bondia bora zaidi kuwahi kutokea katika uzito wake.

Katika michezo ya Majiha ambayo imekuwa ikifuatiliwa na Pambazuko, imeonesha kuwa bondia huyo wa Tanzania huanza kwa nguvu na kasi kubwa katika raundi za awali, lakini hupungua na kuchoka inapofika raundi ya saba na kuendelea.

Mbali na kupungua kwa kasi ya kushambulia, Majiha pia anatakiwa kuwa mwepesi, hasa kukwepa mashambilizi, akijikinga na kujitahidi katika wepesi wa ‘kuchezesha miguu’ (footworks) huku akimuweka mbali mpinzani.

Katika kipindi ambacho Majiha anasubiri kupata mpinzani wake, ni vyema akazidisha mazoezi, kujiepusha na “starehe,” na kusikiliza ushauri wa walimu, wapenzi na kupata muda wa kutazama video - kwa kujifunza zaidi, kutoka kwa mabondia wakubwa na maarufu duniani.





Timu ya taifa ya mchezo wa rugby ya Afrika Kusini, maarufu Springboks, ndiyo mabingwa wa dunia waliotawazwa Oktoba 28, 2023 – baada ya kuibuka washindi dhidi ya wenzao wa New Zealand katika mchezo uliofanyika Uwanja wa Stade de France ulioko jijini Paris. Afrika Kusini sasa ni mabingwa mara nne. Pambazuko linawapongeza kwa ushindi huo. (Picha kutoka Planet Rugby).

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

